# WILAYA YA NAIROBI
# DARASA LA TANO MUHULA WA TATU

PENPLUS NAIROBI

## KISWAHILI

***MUDA Saa 1 Dakika 40***

Mtoto __1__ aliacha mchezo __2__ aliokuwa __3__ na akafuata maneno __4__, __5__ na akatokea __6__ mtoto __7__ __8__. Na akatokea __9__ mtoto __10__ __11__ wote darasani __12__. Kwa hivyo mtihani __13__ yeye ndiye __14__ wa kwanza.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. ule | B. yule | C. wale | D. vile |
| 2. | A. yako | B. zake | C. wake | D. lake |
| 3. | A. anayo | B. nalo | C. nako | D. nao |
| 4. | A. aliyokuwa | B. alikuwa | C. alizokuwa | D. alilokuwa |
| 5. | A. akifuata | B. akizifuata | C. akiyafuata | D. akazingatia |
| 6. | A. akasingatia | B. akashikia | C. akazungukia | D. akazingatia |
| 7. | A. aliambiwa | B. alipoambiwa | C. alizoambiwa | D. aliyoambiwa |
| 8. | A. yake | B. wake | C. ake | D. wako |
| 9. | A. kua | B. kukua | C. kuwa | D. kukuwa |
| 10. | A. mhodari | B. hodari | C. mbora | D. mshujaa |
| 11. | A. kumliko | B. kuwaliko | C. kuliko | D. kukiliko |
| 12. | A. huo | B. hilo | C. hiyo | D. humo |
| 13. | A. mwao | B. lao | C. yao | D. nao |
| 14. | A. ulikuja | B. ulipokuja | C. uliyekuja | D. ilipokuja |
| 15. | A. akakuwa | B. akakua | C. akawa | D. akuwe |

***Kutoka swali 16-30 jibu kulingana na maagizo.***

16. Maxim hutembea kuelekea shuleni asubuhi kivuli chake kikiwa nyuma yake. Je, Shule yao ni upande gani?
A. Mashariki
B. Kaskazini
C. Kusini
D. Magharibi

17. Andika wingi wa "Rafiki yangu ana ugonjwa wa kifua kikuu?"
A. Rafiki zetu wana ugonjwa wa kifua kikuu
B. Marafiki wetu wana magonjwa ya vifua vikuu
C. Rafiki zangu wana magonjwa ya vifua vikuu
D. Rafiki zangu wana ugonjwa wa kifua kikuu

18. Njoki alifika shuleni saa 3:15 asubuhi. Huu ni wakati wa saa.
A. Tisa na Robo
B. Tatu na Robo
C. Nne Kasorobo
D. Kumi Kasorobo

19. Mwangaza mkali wakati wa mvua huitwa:-
A. Masika
B. Radi
C. Umeme
D. Jua

20. Msimu wa mvua ndogo ndogo au mvua fupifupi huitwa:-
A. Vuli
B. Masika
C. Kipupwe
D. Kiangazi

21. Neno pua liko katika ngeli gani?
A.A-WA
B.YA-YA
C. I-ZI
D. U-U

22. ***Chagua jibu sahihi.***
Udogo wa kichwa ni:-
A. Kijikichwa
B. Kakichwa
C. Kijichwa
D. Kijijichwa

23. Neno sahihi linatokana na kitenzi ruka ni:-
A. Rushua
B. Rusha
C. Rukisha
D. Rukishisha

24. Badilisha kiashiria kisisitizi "Yayo Hayo" kuwa kiashiria takriri
A. Hiyo hayo
B. Hayo Hayo
C. Haya hayo
D. Hayo Yayo

25. Tumia alama sahihi ya uwakifisha. " Kumbe juma ni mwizi _________ "
A.(?)
B. (")
C. (!)
D. (.)

26. Zaibaki na Zuhura ni aina za_________
A. Nyota
B. Dunia
C.Sayari
D. Anga

27. ***Kanusha sentensi hii:-***
Mama alienda sokoni
A. Mama hakuenda sokoni
B. Mama hajaenda sokoni
C. Baba amerundi sokoni
D. Mama haendi sokoni

28. $^{3}/_{5}$ huitwa _____________
A. Humusi
B. Humusi tatu
C. Humusi humusi
D. Tatu juu ya tano

29. Dada ya mama yako ni
A. Halati
B. Mjuu
C. Binamu
D. Kilembwe

30. Niliwavua samaki tisa. Watatu wakaoza. Waliosalia ni:-
A. Thuluthi mbili
B. Tusui saba
C. Thumuni mbili
D. Thuluthi moja

***Soma habari hii kisha ujibu maswali kutoka 31-40.***

Hebu tutafakari kinachotokea katika birika au chungu chenye maji yanayochemka. Kwanza yale mjai yaliyo chini, yaani yaliyo karibu zaidi na moto, hupata joto jingi. Mara yachemkapo huwa mepesi kuliko yasiyochemka, kwa hivyo hupanda juu katika birika au chungu na yale maji ya juu yaliyo baridi huteremka chini. Baadaye kidogo, maji yale yaliyoteremka chini hupata joto zaidi, nayo hupanda juuu. Yale ya juu yaliyopoa kidogo huteremka chini tena. Basi, yaliyo katika birika au chungu huzungukazunguka ndani yake.

Tena hatuma budi kukumbuka kuwa maji yanapochemka au kupata joto hutanuka kama vitu vingine vinavyotanuka na kwa hivi, yanatakia nafasi zaidi. Ukikitwaa chungu kilichojaa maji pamoni na kukifunika kisha ukiinjike motoni, mara maji yachemkapo, mengine yatafurika na kumwagika kifuniko kikiwa kimekazwa sana. Basi maji yaliyochemka yatakitoa kifuniko kwa nguvu yakitafuta nafasi zaidi. Utayaona mapovu juu ya maji yachemkayo. Kwani maji mengine yamegeuka mvuke unaopaa kwa nguvu na kuingia hewani.

**31.** Maji hupitia hutua zipi hadi kuwa mvuke?
- A. Huchemka, hutanuka, hupaa hewani na kuwa mvuke
- B. Hutanuka, huchenka, hupaa hewani na kuwa mvuke
- C. Hupaa hewani, huchemka, hutanuka na kuwa mvuke
- D. Kuwa na mvuke

**32.** Maji yanapochemka, yaliyo karibu zaidi na moto_____
- A. Hugeuka hewa na kupaa angani
- B. Huchemka kwanza na hatimaye huyachemsha yaliyo juu
- C. Huwa mepesi na kupanda juu kuyapisha yasiyochemka yateremke chini
- D. Hutanuka na kusababisha yaliyo juu yamwagike

**33.** Chagua kauli isiyo sahihi.
- A. Mvuke ukikutana na hewa baridi hauwezi kuganda na kuwa maji tena.
- B. Maji yakichemka huongezeka ujazo
- C. Mvuke ni maji yaliyochemka na kuwa hewa
- D. Maji yaliyochemka ni mepesi kulio yasiyochemka

**34.** Kinachotokea hasa katiaka birika au chungu maji yanapochemka ni:-
- A. Kuchemka, kumwagika na kutanuka.
- B. Mzunguko, kumwagika na mvuke
- C. Mzunguko, kutanuka na mvuke
- D. Mzunguko na mvuke

**35.** Tatafakari ni sawa na:-
- A. Tujihadhari
- B. Tukumbuke
- C. Tuwaze
- D. Tutahayari

**36.** Hatuna budi maana yake ni:-
- A. Tusiweke bidii
- B. Tusijali
- C. Si lazima
- D. Yatulazimu

**37.** Kujaa maji pamoni maana yake ni:-
- A. Maji yaliyochemka
- B. Maji mengi
- C. Maji yaliyojaa mpaka juu
- D. Maji ya kutosha

**38.** Moja kati ya yafuatayo huweza kutokea baada ya kuchemsha maji kwa muda mrefu sana.
- A. Maji yanaweza kuendelea kutanuka na kulipua birika
- B. Maji yote yanaweza kuyeyuka na birika kukauka
- C. Maji yote yanaweza kumwagika na kuuzima moto
- D. Maji yote yanaweza kuchemsha zaidi mpaka yageuke moto

**39.** "Utaona mapovu juu ya maji yachemkayo". Aidha utayaona mapovu kwenye:-
- A. Maji ya kisimani
- B. Maji ya barafu
- C. Maji ya sabuni
- D. Mvuke

**40.** Kichwa mbora kwa habari hii ni:-
- A. Nguvu za mvuke
- B. Mzunguko wa mvuke
- C. Nguvu za maji
- D. Mzunguko wa maji

***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 41-50.***

Mzee mmoja mwanaume akiwa mbioni kasi sana alitokeza machakani palipokuwa karibu, kandokando ya baraste huku amemfuata pofu aliyekuwa vilevile ameshika kasi ajabu kuokoa maisha yake. Huyo mnyama alipofika baraste aliivua kasi mithili ya umeme. Msasi naye maskini hakuhakikisha kama kwamba kulikuwa na magari. Alivuka mbiombio kumfuata huyo pofu aliyekuwa usalamani. alipofika katikati ya baraste kushtuka tu, gari lilikuwa safarini mbio likamgonga dafrao likamrusha juu kishaye akaanguka katikati ya barabara kwa kishindo pu! Dereva bila shaka alikuwa amejaribu awezavyo kumhepa lakini hakufua dafu! Matwana yenyewe ilisita hatua arubaini na mkumbano baina ya mtu na gari hilo uliwagutusha watu waliokuwa karibu na wapita njia nao wakaja gwarideni kushuhudia jambo hilo la kutisha macho. Alipogundua kuwa bado alikuwa akipumbua akaomba msaada wa kumbeba na kumwigiza ndani ya matwana hiyo ambayo sasa ilikuwa imeegeshwa pande zote mbili za baraste. Pindi tu gari likango'a nanga kasi likierea hospitali moja mahususi na mgonjwa wake mahututi, kilomita chache kulikotokea gari lenyewe.

**41.** Povu alikuwa mbioni kuokoa:-
A. Maisha ya wasafiri wa gari lile
B. Maisha ya maskini msasi
C. Maisha yake mwenyewe
D. Maisha yake na ya mzee maskini

**42.** " Wakaja gwarideni .......ina maana gani?
A. Walizunguka gari la dereva
B. Walimzingira Mgonjwa
C. Waliizingira barabara
D. Walimzingira pofu

**43.** Aliyepigwa dafrao ni:-
A. Msasi na Masiwa
B. Masasi na Dereva
C. Msasi wa wasafiri
D. Msasi peke yake

**44.** Dereva aliomba msada kwa:-
A. Walio gwarideri
B. Waliomo garini
C. Walio kando kando na barabara
D. Wapita njia

**45.** Mzee huyo mwanaume alitaka ________
A. Kupanda garii
B. Kujiunga na wapita njia
C. Kumwua pofu
D. Kusalimika

**46.** Mnyama:-
A. Alijiokoa kwa mbio
B. Alinusurishwa na gari
C. Waliokolewa na wapita njia
D. Walinusurishwa na maskani mzee

**47.** Dereva hakufua dafu:-
A. Kumwua mzee
B. Kumhepa
C. Kuliegesha gari
D. Kumnusuru maskini msasi

**48.** Zahanati maalum hiyo ilikuwa:-
A. Upande wa nyuma kutoka mahari pa ajali
B. Upande wa mbele kulikotokea gari lile
C. Upande ambao haukueleza katika hadithi
D. Karibu na barabara

**49.** "Aliyekuwa usalamani" ina maana ya:-
A. Aliyekuwa na mwindaji
B. Aliyeponyoka
C. Aliyevuka baraste
D. Aliyesalimika na waliomo garini

**50.** Majeruhi ________
A. Alikuwa dereva
B. Walikuwa gwarideni
C. Alikuwa mwindaji
D. Alikua pofu